MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Uhakiki wa Masuala ya Kitamaushi Katika Riwaya ya *Safari ya Lamu*

John Swala*, Judith Khasoa

*Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi, Shule ya Elimu, Chuo Kikuu cha Kibabii, Bungoma, Kenya*

**IKISIRI**

Waandishi wa riwaya huwasilisha masuala mbalimbali katika kazi zao. Mojawapo wa masuala haya ni masuala ya utamaushi wa wahusika. Hali ya kitamaushi huwasilishwa wakati wahusika hujiuliza kuhusu maisha, kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu duniani na kifo cha binadamu kama suluhisho la matatizo ya binadamu duniani. Tafiti za awali zilishughulikia utamaushi kama nadharia ya uhakiki na uchambuzi wa kazi za kifasihi. Ili kuelewa suala la kitamaushi zaidi, ni muhimu masuala ya kitamaushi yahakikiwe zaidi katika kazi zinazowasilisha masuala haya kiundani. Hili ndilo pengo lililochochea uandishi wa makala hii. Madhumuni ya makala hii ni kuhakiki masuala ya kitamaushi katika riwaya ya Safari ya Lamu. Nadharia ya utamaushi ilitumiwa kuwasilisha na kuchanganua data. Riwaya ya Safari ya Lamu ilichaguliwa kimaksudi kwa sababu mwandishi alitumia wahusika waliotamauka katika kuwasilisha maudhui yake. Huu ulikuwa utafiti wa maktabani ambapo data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya upekuzi wa yaliyomo katika riwaya husika. Kwa sababu data zilikuwa za kithamano, mbinu ya kimaelezo ilitumiwa katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Makala hii ilibainisha kuwa masuala ya kitamaushi kama vile kifo, ndoa na maisha yamewasilishwa katika riwaya husika. Makala hii ni muhimu sana kwa wachanganuzi wa riwaya kwa sababu mbinu na nadharia za uchanganuzi wa riwaya zilishughulikiwa katika makala hii.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Utamaushi,
Udhanaishi,
Riwaya

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 06 Juni 2024
Tarehe ya Kurekebishwa: 30 Julai 2024
Tarehe ya Kukubalika: 10 Oktoba 2024
Mtandaoni: 28 Machi, 2025

## 1. Utangulizi

Suala la utamaushi limeelezwa kwa namna mbalimbali na wataalam tofauti wa fasihi. Tafiti nyingi zilizofanywa katika utamaushi zimeshughulikia suala la utamaushi kama nadharia ya uhakiki wa kazi za fasihi. Kulingana na TUKI (2014), kutamauka ni hali ya kukosa matumaini au kukosa tamaa ya kupata kitu. Kulingana na maelezo haya, kutamauka ni kukata tamaa. Simiyu (2013) anaeleza kuwa utamaushi ni falsafa inayoeleza kuhusu maisha ya mwanadamu duniani. Ni mtazamo unaomwezesha binadamu kuelewa maana ya maisha na kifo kama suluhisho la matatizo ya binadamu duniani. Malugu & Jjingo (2024) wanaeleza kuwa suala la utamaushi hujikita katika kueleza maana ya maisha pamoja na kiini cha maisha kwa binadamu. Maisha ya binadamu huwa na mambo mengi mabaya ambayo humfanya kukata tamaa katika maisha yake. Wamitila (1998) ameeleza kuwa maisha ya binadamu duniani yana mateso mengi. Anaeleza kuwa wahusika wengi katika kazi za Euphrase Kezilahabi wamekata tamaa kwa sababu ya mateso wanayopitia katika maisha yao.

Waandishi wa kazi za sanaa huwasilisha ujumbe wao kwa kutumia mbinu mbalimbali. Mbinu hizi hulenga kuwasilisha maudhui kwa njia itakayoeleweka na hadhira mahususi pekee. Ujumbe hulenga hadhira mahususi na kuipuuza hadhira ambayo haijakusudiwa kupata ujumbe uliomo kwenye kazi husika. Maudhui na ujumbe katika kazi za kifasihi huwasilishwa kupitia kwa matukio yanayotendwa na wahusika au kutendeka kwa wahusika. Waandishi wa kazi za fasihi huwasilisha matukio mengi kama vile ya kimuyemuye, matukio ya kihasiliajabu na matukio ya kitamaushi. Kulingana na Chimerah (2021) mwandishi Euphrase Kezilahabi ndiye maarufu zaidi katika kuwasilisha matukio ya kitamaushi katika kazi zake kama vile Rosa Mistika na Kichwa Maji. Matukio ya kitamaushi huwa vifo au mauti, njaa, ubakaji, matumizi mabaya ya dini na mengine mengi. Kuna waandishi wengine ambao pia wamefuata mkondo huu wa kitamaushi. Katika kazi yake ya Safari ya Lamu, mwandishi John Habwe amewasilisha matukio ya utamaushi ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Kwa hivyo makala haya yalinuia kuhakiki matukio ya kitamaushi katika riwaya ya Safari ya Lamu iliyoandikwa na John Habwe.

Utamaushi hujishughulisha na vipengele muhimu sana katika maisha ya binadamu. Maisha ya binadamu wengi huzungukia masuala kama vile Mungu kama muumba wa kila kitu duniani, maisha ya binadamu

* Mwandishi Mkuu. Simu: +254706468094; Barua Pepe: johnswala@gmail.com
Mhariri: Pamela Ngugi, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
Nukuu: John S., Judith K. (2024). Uhakiki wa Masuala ya Kitamaushi Katika Riwaya ya *Safari ya Lamu*. Jarida la Kiswahili Sanifu 2(2025), 1 – 7.

© 2025 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

duniani na baadaye kifo. Tafiti nyingi za awali zilionyesha kuwa mwandishi Euphrase Kezilahabi ndiye maarufu sana katika uandishi wa kazi za kitamaushi. Hivi majuzi, kuna baadhi ya watafiti kama vile Mui na wenzake (2023) na Muli (2024) wanaodai kuwa kazi za John Habwe kama vile Paradizo na Maisha Kitendawili pia zina vipengele vya kitamaushi. Katika kupitia tafiti za awali, mtafiti wa kazi hii hajakumbana na utafiti ulioonyesha hali za kitamaushi katika riwaya ya Safari ya Lamu iliyoandikwa na John Habwe. Hili ndilo pengo lililonuiwa kujazwa katika utafiti huu ili kuongeza maarifa kwa kazi za awali katika taaluma ya nadharia ya utamaushi.

## 2. Mapitio ya Maandishi

Kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu utamaushi katika fasihi hasa riwaya ya Kiswahili. Malugu & Jjingo (2024) alihakiki mbinu za kukabiana na utamaushi jinsi ilivyojitokeza katika nyimbo za Diamond Platnumz na kubainisha kuwa mwimbaji huyu anachukulia maisha kuwa mafupi sana. Ili kukabiliana na maisha ambayo ni mafupi, ni vyema wanadamu wafurahi maisha. Ugumu wa maisha haumruhusu mwanadamu kuwa na msongo wa mawazo. Mwimbaji huyu anaeleza kuwa mapenzi ndicho chanzo cha msongo wa mawazo. Kwa hivyo binadamu hastahili kujiumiza sana kwa kufikiria mambo ambayo hawezi kuyadhibiti. Binadamu anaweza kupata utulivu wa akili kwa kunywa pombe na kukaa na watu vizuri. Suala la maisha katika utamaushi limejadiliwa na Simiyu (2024) kuwa ni muundo duara. Maisha ni mzunguko tu wa watu. Wale wanaoshi hufa na kuzaliwa tena katika jamii. Simyu (2024) alijadili suala la kifo katika maombolezi ya Ken Walibora na kubainisha kuwa Mungu ndiye chanzo cha maisha ya binadamu wote duniani. Mungu huwaondoa binadamu duniani wakati wowote anapotaka na kazi yake Mungu haina makosa. Kulingana na hali ya kitamaushi, ni binadamu aliyemuumba Mungu ili kuelezea hali za Maisha kama vile kifo. Utafiti wa Fuluge (2022) alihakiki mchakato wa kujiua kwa mitazamo ya kinadharia na kubainisha kuwa binadamu anaweza kujiua kwa sababu ya kukata tamaa, misukosuko ya kimaisha, mateso na maangaiko katika maisha. Utafiti wa Fuluge (2022) ulibainisha kuwa kiini cha mhusika mkuu katika riwaya ya Rosa Mistika kujiua ni kuachwa na mpenzi wake. Tukio la kuachwa na mpenzi linasababisha kukataa tamaa kwa sababu ya usaliti wa kimapenzi.

Wangari (2019) alihakiki hali ya kukata tamaa kwa mujibu wa kitamaushi. Anakiri kuwa binadamu hukata tamaa kimaisha kwa sababu mbalimbali. Sababu hizi ni kama kukosa kazi, ugumu wa maisha unaosababishwa na hali za kiuchumi na ajali za barabarani zinazotokea kila mara. Uhakiki wake ulibainisha kuwa matizo yanayomkumba binadamu duniani husababishwa na binadamu mwenyewe. Poyi (2021) alihakiki ubwege katika diwani ya Kichomi na kubainisha kuwa ubwege hutumiwa kuelezea hali ya maisha. Alieleza kuwa ubwege ni maudhui katika utamaushi. Katika hali hii ubwege hueleza kukosekana kwa maana katika maisha ya binadamu. Maisha yameelezwa kuwa ni hali inayotokea tu bila kukusudia. Binadamu hujipata tu duniani bila kukusudia. Katika kukosa kuelewa maana ya maisha na umuhimu wake duniani, binadamu hukata tamaa maishani. Kukata tamaa kunatokana na hali kuwa kujitungia maana ya maisha ni kazi ya upuzi ambayo haistahili kupewa nafasi katika fikra za binadamu. Chimerah (2021) alihakiki suala la utamaushi kama maudhui katika riwaya za Kitu Kidogo Tu! Na Harusi ya Wendawazimu na kubainisha kuwa miongoni mwa masuala mengine katika maudhui mapana ya utamaushi, suala la ndoa limejitokeza kwa mapana. Kulingana na utafiti wake, ndoa katika jamii zilizotamauka ni taasisi ambayo haina heshima. Katika riwaya za Kitu Kidogo Tu! Na Harusi ya Wendawazimu, vijana hawajishughulishi na ndoa kwa sababu itawanyima uhuru wao wa kuishi jinsi wanavyotaka.

Muli (2024) anaeleza kuwa kuna utamaushi wa kidini katika riwaya za *Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea*. Muli anaeleza kuwa kuna masuala ya kidini ambayo yanatamausha vijana katika riwaya hizi. Vijana wanatamauka katika dini kwa sababu kuna mipango ya kando ambapo watu walio katika ndoa wana wapenzi wengine nje ya ndoa zao. Micheal ambaye ni mchungaji wa kanisa, ana mpenzi wan je kwa jina Patricia ilhali ana mke wake wa ndoa kwa jina Lydia. Jambo jingine linalotamaushwa ni kutoelewana katika madhehebu mbalimbali. Kutoelewana kunatokea kwa sababu kuna washiriki ambao hawajapewa nafasi za uongozi katika dini wanakoshiriki. Hizi ni baadhi ya hali ambazo zinatamausha vijana katika riwaya za Paradiso na Kidagaa Kimemwozea. Kwa sababu ya kutamauka, vijana na wahusika wengine wanatafuta miungu wengine wa kuabudu. Mwalimu Majisifu Maji Marefu anaanza kuabudu miungu wengine kwa sababu ya kukata tamaa. Kwa hivyo utafiti huu ulitumia maelezo ya Muli (2024) katika kueleza hali za kitamaushi katika riwaya ya *Safari ya Lamu*.

### 2.1. Nadharia ya Utamaushi

Uandishi wa makala hii uliongozwa na nadharia ya utamaushi. Nadharia hii ilichaguliwa kimaksudi kwa sababu inaoana na mada ya makala hii. Dhana ya utamaushi pia huweza kurejelewa kama udhanaishi. Kulingana na Chimerah (2021) dhana ya utamaushi inahusishwa na Ki-Deni Soren Kierkegaard (1849). Kulingana na mtaalam wanaoshikilia mtazamo wa kitamaushi, dini haiwezi kutatua matatizo ya binadamu duniani. Matukio ya kitamaushi huwafanya wahusika kujiuliza kuhusu maana ya maisha na yana maana gani kwa maisha ya mwanadamu duniani.

Malungu & Jjingo (2024) wanaeleza kuwa nadharia ya utamaushi ilizuka wakati wa vita vya pili vya dunia katika nchi za Kimagharibi ambapo kulikuwa na mateso mengi. Katika wakati huu kulikuwa na mateso mengi duniani. Mateso haya yaliwafanya binadamu kukata tamaa. Kulishuhudiwa vifo vingi vya watu walikuwa vitani. Kulikuwepo na mporomoka wa maadili. Kutokana na ugumu wa maisha binadamu walipoteza imani maishani. Wengi wao walizua imani kuwa Mungu alikuwa amekufa kwa sababu angekuwepo hangeruhusu binadamu kuteseka maishani. Maisha yalikosa maana

katika kipindi hiki. Binadamu hawakuona malengo ya kuishi kwa sababu hatma ya maisha ilikuwa kifo.

Kulingana na Simiyu (2013) utamaushi ni mtazamo unaoangaza maisha ya binadamu na dhiki anazopitia akiwa duniani. Watamaushi hujikita katika suala la kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu. Wanashikilia mtazamo kuwa ni binadamu ndiye aliyemuumba Mungu ili kuweza kuelewa dunia anamoishi. Wanaoshikilia mtazamo huu hawaoni maana ya kuwa makini katika maisha kwa sababu hatima ya binadamu duniani ni kifo. Kwa hivyo maisha ya binadamu duniani ni Kifo cha polepole. Hii inamaana kuwa maisha hayana maana yoyote. Binadamu anastahili kuishi maisha jinsi yalivyo akisubiri kifo. Katika mtazamo wa matukio ya kitamaushi, kuna pia suala la ndoa. Swali ni je kuna nini katika ndoa? Ndoa haina furaha wala raha yoyote na kama ipo, basi ni kidogo sana. Kila mtu ana wakati wake wa kutenda atakayo na wakati wake ukiisha, basi binadamu anastahili kutoka jukwaani na kuwaachia wengine. Binadamu anastahili kung'ang'ana katika maisha yake bila kutarajia msaada wowote kutoka kwa watu wengine kwa sababu maisha yamejaa huzuni na dhiki. Suluhisho ya dhiki na huzuni katika maisha ni kifo.

Chimerah (2021) anaeleza kuwa utamaushi ni falsafa inayoeleza uhusiano uliopo kati ya binadamu na Mungu. Nadharia hii pia huchunguza nafsi ya binadamu katika ulimwengu anamoishi. Binadamu haishi kwa nguvu zake mwenyewe bali hutegemea nguvu zilizomuumba. Katika matatizo anayopitia binadamu, ndipo binadamu huyo hukimbilia nguvu za kiroho ambazo zina nguvu zaidi. Hali hii ndiyo huzua suala la kuwepo kwa Mungu. Binadamu hishi maisha ya hofu ili asimkosee Mungu. Iwapo atafanyia Mungu makosa, binadamu huomba msamaha ili awe na utulivu wa moyo. Binadamu anastahili kuwa na lengo katika maisha yake na ikiwa atasahau malengo yake maishani na kukimbilia raha, basi ataishi maisha yasiyo na maana.

Nadharia ya utamaushi ina mihimili ifuatayo;
**Binadamu**. Wananadharia ya utamaushi hujishughulisha na uhusiano ulipo baina ya binadamu na Mungu. Wao wanakisia kuwa ni binadamu ndiye aliyemuumba Mungu ili kukabiliana na matatizo ya dunia.
**Suala la Mungu**. Watamaushi hushughulikia kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu. Wanakisia kuwa Mungu aliumbwa na binadamu ili kutatua matatizo yanayomkumba duniani.
**Kifo**. Kifo ni suluhisho la matatizo yote amabayo yanamkumba bindamu duniani. Kifo humpa binadamu hali ya kujituliza.
**Ndoa**. Ndoa haina raha yoyote, na kama kuna raha katika ndoa, basi ni kidogo sana.
**Maisha**. Maisha hayana maana yoyote kwa binadamu. Maisha ni kifo cha polepole. Maisha yanavyosonga, ndipo binadamu husonga karibu na kifo chake.

Kulingana na makala hii, iliyotajwa ni baadhi ya mihimili ya nadharia ya utamaushi. Kwa hivyo uandishi wa makala hii ilitumia mihimili ya suala la kifo, ndoa na maisha katika kuhakiki masuala ya utamaushi katika riwaya ya Safari ya Lamu.

## 3. Njia na Mbinu za Utafiti

Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo kwa sababu data zilikuwa za kithamano. Kulingana na Ogechi (2024) muundo wa kimaelezo huweza kutoa maelezo kuhusu masuala ya kidhahania. Muundo huu ulifaa kwa sababu masuala ya kitamaushi ni masuala ya kidhahania katika fasihi. Utafiti ulifanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya upekuzi wa yaliyomo. Wilson (2011) anaeleza kuwa upekuzi wa yaliyomo hutumiwa katika utafiti kukusanya data kutoka kwa matini. Mbinu hii ilifaa katika utafiti huu kwa sababu Safari ya Lamu ni matini yaliyoandikwa. Ni riwaya moja tu ndiyo iliyotumiwa kuwasilisha riwaya zingine zilizo na hali za kitamaushi. Riwaya ya Safari ya Lamu pia imetumiwa kuwakilisha riwaya zingine zilizoandikwa na John Habwe. Maktaba ni muhimu sana katika utafiti wowote kwa sababu ndipo mahali panapopatikana vitabu, makala na majarida kuhusu taaluma mbalimbali (Buliba na wenzake 2014). Kwa hivyo mtafiti wa makala hii alijikita maktabani kwa sababu ya ukwasi wake wa makala muhimu ya utafiti huu.

Data zilikusanywa kutoka kwa riwaya ya Safari ya Lamu (Habwe 2011) kwa kutumia mbinu ya upekuzi wa yaliyomo. Mtafiti alisoma riwaya na kudondoa hoja zinazowasilisha matukio ya kitamaushi kwa minajili ya uchanganuzi na uwasilishaji. Uchanganuzi na uwasilishaji uliongozwa na mihimili ya nadharia ya utamaushi. Riwaya hii ilichaguliwa kimaksudi kwa sababu inawasilisha hali za kitamaushi ambazo ziliwakumba baadhi ya wahusika. Nyimbili & Nyimbili (2024) wanaeleleza kuwa mbinu ya usampulishaji ya kimaksudi ni mbinu ambayo mtafiti huchagua watafitiwa ambao anajua wana data ambayo anahitaji katika utafiti wake. Kwa sababu data zilikuwa za kithamano, mbinu ya kimaelezo ilitumiwa katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Buliba na wenzake (2014) wanaeleza kuwa mtindo wa kimaelezo hutumiwa katika kuwasilisha na kuchanganua data zinazohusu lasihi, lugha na Isimu. Wanaeleza kuwa data katika nyanja hizi hazina mambo mengi changamano na mambo huelezwa jinsi yalivyo bila kubadilisha vibadilishi.

## 4. Utamaushi katika Riwaya ya Safari ya Lamu

Utafiti ulibaini masuala mbalimbali katika riwaya ya Safari ya Lamu. Sehemu ifuatayo inabainisha masuala hayo na kutoa mifano katika riwaya.

### 4.1. Suala la Maisha

Kulingana na nadharia ya utamaushi, maisha hayana maana na pia hayana raha. Wamitila (1998) anaeleza kuwa wahusika wengi katika kazi za Euphrase Kezilahabi wamekata tamaa maishani kwa sababu ya mateso wanayoyapitia katika maisha yao. Hali hii ya kutamauka inajitokeza katika riwaya ya Safari ya Lamu. Mohamed anaonyesha dalili za kutamauka maishani. Anapoona Musa amepata barua ya kuenda likizoni, anakosa matumaini ya kuishi kwa sababu wafanyikazi wa tabaka la juu wanapewa likizo na wengine kama yeye hapewi likizo. Musa anampa matumaini kuwa siku moja mambo yatabadilika pale kazini na yeye pia atapata fursa ya kuwa na likizo. Hali hii inabainika katika dondoo 1:

> “Santa Mariaah!” Nilisema kwa furaha.
> “Kuna nini?” Mohamed aliuliza kwa mshangao.
> “Livu Baba,” nilisema huku nimesimama.
> “Heri nyinyi mnaokwenda,” Alisema Mohamed akionyesha kutamauka maishani.
> (Dondoo 1, uk.3).

Dondoo 1 ni mazungumzo kati ya Musa na Mohamed yanayoonyesha kuwa Mohamed ametamauka maishani na hana matumaini tena kwa sababu ya tabaka lake la chini kazini. Hili ni suala la kitamaushi kwa sababu Mohamed amekata tamaa maishani kwani hakuna kizuri kinachokuja kwake. Yeye ni miongoni mwa watu ambao wanastahili kuwa kazini wakifanya kazi bila kupumzika. Mohamed ni mfanyikazi ambaye amechoka na hana tamaa na chochote maishani. Hali hii inaoana na mhimili wa nadharia unaosema kuwa maisha hayana maana kwa binadamu.

Ajali iliyotokea manyani ni dhihirisho kuwa maisha hayana maana yoyote kwa binadamu. Dereva na tuniboi wa trela waliaga dunia. Ajali hiyo pia ilichukua maisha ya bwana mmoja wa haiba. Mifuko yake ilikuwa na pesa nyingi zilizopangwa katika mabunda. Shajara yake pia ilionyesha kuwa mtu huyu alikuwa na mipango mingi sana ya maisha yake kama inavyodhihirika katika dondoo 2.

> *Nilijongea karibu na maiti aliyeonekana mtu wa haiba. Mifuko yake ilionekana kuwa na pesa. Mabunda ya note labda shajara yake ilikuwa hapo hapo karibu naye. Katika ukurasa mmoja alikuwa amejipangia shughuli za miezi miezi miwili ijayo. Katika tarehe moja, bwana huyo alikuwa amejipangia kwenda Marekani kwa safari ya kibiashara. Katika tarehe nyingine alikuwa amejipangia hafla ya binti yake. Shajara ilijaa kila Ukurasa. Nilianza kuwaza kuhusu hadaa ya maisha. Mwanadamu anajiona ana uwezo wa kuyadhibiti maisha yake lakini jambo dogo linapotokea anaonekana kushindwa kabisa kuyatekeleza haya mambo. Mwanadamu awapo mzima, anayaringia maisha, kumbe si lolote si chochote.*
> (Dondoo 2, uk.19-20)

Dondoo 2 ni dhihirisho kuwa maisha ya binadamu hayana maana yoyote kwake. Binadamu ana uwezo wa kupanga kila kitu katika maisha yake lakini kifo huweza kukatiza shughuli zote ambazo binadamu amepanga. Kifo ni mojawapo wa mihimili ya nadharia ya utamaushi. Kulingana na nadharia hii kifo humuondolea binadamu matatizo na pia kifo hakiwezi kuepukika. Huyu bwana alikuwa amepanga shughuli nyingi lakini hakuweza kuzitekeleza kwa sababu kifo kilikatiza maisha yake. Pesa pia si muhimu sana katika maisha ya binadamu. Pesa haziwezi kutumiwa kununua maisha kwa sababu huyo bwana amefariki lakini hakuweza kuzuia kifo. Kulingana na Malungu & Jjingo (2024) binadamu anastahili kufurahia hali ya maisha jinsi yalivyo kwa sababu binadamu hana udhibiti wowote kwa maisha yake. Binadamu hastahili kujishughulisha na mambo ambayo yatakuja baadaye kama bwana huyu aliyefariki. Yeye alikuwa na pesa ambazo hazijamsaidia kujipa furaha bali amekufa kwa ajali na kuziacha.

Maisha ni magumu na binadamu wanatumia mbinu mbalimbali kufumbua riziki. Ili kuyaelewa maisha ya binadamu duniani, Binadamu alimuumba Mungu ili aweze kujibu maswali yasiyokuwa na majibu. Binadamu hufanya lolote ili kupata riziki yao. Kuna wengine ambao huua ili kupata riziki yao. Wote hawa husahau kuwa mwandamu ana jaza yake kwa Mungu ambaye binadamu mwenyewe alimuumba ili kuyaelewa maisha. Kwa hivyo lolote ambalo Mungu amepanga, lazima litatokea. Hali hii inaoana na makala ya Simiyu (2024) anapoeleza kuwa binadamu hawezi kuyaendesha maisha yake mwenyewe asipomtegemea Mungu. Ni Mungu ndiye huwapa binadamu maisha na ni yeye tu ndiye huweza kuchukua maisha ya binadamu wakati wowote anavyopenda.

Binadamu hastahili kutarajia msaada wowote kutoka popote. Nadharia ya utamaushi humwongoza binadamu kuwa asitarajie msaada wowote kutoka kwa watu. Hii ndiyo maana Musa anapofika Mombasa, hatarajii msaaada wowote kutoka kwa mtu mwingine ingawa Kombo alikuwa amemwambia kuwa atamsaidia kupata mwelekeo wafikapo Mombasa. Musa anajua vizuri kuwa Kombo ni wa siku hiyo tu kwa vile hatakuwa na yeye muda wote katika maisha yake. Musa pia alielewa kuwa binadamu hutoa ahadi za usaidizi lakini wakati wa kusaidia unapowadia, wao hujipa shughuli zao.

Binamuye Musa kwa jina Petro alichukia maisha baada ya kupata ugonjwa ambao hakuna daktari aliyekuwa na uwezo wa kuutibu. Hili ni suala la kifo katika nadharia ya utamaushi kuwa ni kitulizo cha matatizo yanayomkumba binadamu katika Maisha yake. Ugonjwa huo ulimfanya yeye kukonda sana ndipo akachukia maisha na wanawake. Ugonjwa huo ulimfanya Petero kuwa radhi kufa. Hii ina maana kuwa alikuwa amekata tamaa ya maisha ndiposa akaona ni vyema afe ili kujiondolea shida ya ugonjwa ambao ulikuwa umemsonga. Ugonjwa ulimfanya kuamini kuwa maisha hayakuwa na maana kwa sababu alikuwa akilia kila wakati. Kulingana na Wangari (2019), binadamu hukata tamaa katika maisha kwa sababu ya matatizo yanayomkumba kila siku. Matizo haya ni kama njaa, uchumi na kukosa kazi. Kama Petero, binadamu yeyote anaweza kukata tamaa katika maisha kwa sababu ya ugonjwa ambao hauwezi kutibiwa.

> *Maisha kweli ni kitendawili. Ni vipi mwendawazimu mmoja alijiona bora kuliko mwendawazimu mwingine? Ni vipi mwendawazimu atakuwa na utashi kama huo?*
> (Dondoo 3: uk 70)

Dondoo hili linaashiria maana halisi ya maisha kulingana na nadharia ya utamaushi. Kulingana na Musa ambaye ni msimulizi katika riwaya ya Safari ya Lamu, maisha ni kitendawili. Maisha hayaeleweki na binadamu yoyote. Hii ni baada ya kuwaona wendawazimu wawili wakitaka kuchumbiana. Wanataka kuchumbiana kwa sababu wao pia ni binadamu na wana mahitaji yote ya kibinadamu na ya kimwili. Kinachoshangaza ni kuwa mwendawazimu mmoja anajiona bora kuliko mwendawazimu mwingine. Kunatokea wakati ambapo mwendawazi mmoja anamwita mwendawazimu mwenzake mwendawazimu. Hii ni hali ambayo huwapata binadamu wa kawaida ambao huona tatizo la wenzao bila kuona matatizo yao wenyewe.

Binadamu hung'ang'ania maisha na kutafuta vitu vingi ambavyo haviwezi kumsaidia katika maisha yake. Maisha ni kama umande wa asubuhi ambao hukauka baada ya jua kuwaka na kuukausha. Kulingana na Musa, Petero alikuwa amenunua gari la aina ya Toyota na pia kujenga nyumba nzuri lakini vitu hivi havikuweza kuzuia kifo. Maisha ya binadamu ni kama umande wa asubuhi kweli. Ukadhani yako kumbe hayapo. Petero alikuwa amenunua gari la aina ya Toyota na kujenga nyumba mjini Kisumu. Yote haya ameyaacha. (Dondoo 3, uk 80)

Dondoo 3 linadhirisha kuwa mali waitafutayo binadamu katika maisha yao haina maana yoyote kwa sababu wataiwacha hapa duniani. Baada ya kifo, Petero hatatumia gari wala hataishi katika nyumba yake aliyoijenga mjini Kisumu. Kwa hivyo kifo ni hatma ya maisha na pia huonyesha mwisho wa vyote avitafutavyo mwandamu duniani.

Semi nyingi zilizoandikwa katika maleso ya wanawake wa Lamu ni zile za kukosha maisha na mtazamo wa maisha. Maimuna alipopewa nafasi ya kuchagua leso alipendalo, alichagua leso lenye msemo maisha ni muamana. Kulingana na TUKI (2014), muamana ni hali ya kuaminiana. Hali hii inaashiria maisha ya Musa na Maimuna ambao wamekutana muda mfupi uliopita lakini kila mmoja wao ana imani na mwenzake. Musa anamwamini Maimuna hadi amempa fursa ya kuchagua leso na yeye kulilipia.

Nduguye Musa, Simba ametamauka na maisha. Katika familia yake ni yeye tu aliyesoma hadi Chuo kikuu na kupata shahada ya elimu ya kilimo cha ufugaji. Kufikia sasa amepita miaka kumi bila kupata kazi wala kibarua. Hali ya msongo wa mawazo imemfanya anataka kuruka akili. Taswira ya maisha yake yanaonyesha kuwa yeye si timamu tena kwa sababu haogi na nywele zimemtimka. Alipewa elimu ambayo haijamsaidia katika maisha yake. Viongozi ambao walistahili kumpa kazi sasa ni wao tu ndio wana kazi zaidi ya tano. Kinachomuumiza akili sana ni kuwa wale ambao hawakusoma ndio wana pesa na kazi za hadhi za juu nchini. Elimu kwa kawaida inastahili kumpa mtu hadhi ya juu na maisha mazuri lakini kwa kijana huyu Simba imekuwa kinyume. Anataka kurukwa na akili kwa sababu haoni maana ya kuishi tena. Aliambulia patupu baada ya kufanya bidii maishani lakini hakufanikiwa. Kwa hivyo bidii maishani si lazima itoe mtokeo mema. Kulingna na Wangari (2019), ukosefu wa kazi husababisha hali ya kukata tamaa katika maisha ya binadamu. Dondoo hili linaonyesha athari za ugumu wa maisha ambao umetokana na ukosefu wa kazi. Kazi hazipatikani kwa sababu ya ufisadi serikalini. Vijana wamekumbwa na msongo wa mawazo na sasa wanatumia madawa ya kulevya. Hali hii imesababisha wengi wao kuwa majambazi na kuwanyang'anya wananchi chochote wanachopata.

Kifo humleta mwanadamu raha. Kulingana na Musa baadaya ya kufikiria maisha ya Kiboko, maisha hayana raha. Raha hupatikana ahera. Kwake raha ni kitu ambacho hakipo. Raha ni mazigazi tu. Kulingana na nadharia ya utamaushi, raha iko mbali sana na binadamu. Binadamu anapofikia raha, raha husonga mbele zaidi. Maisha yenyewe hayana raha yoyote. Dondoo 4, linadhihirisha hali hii.

> *… nilijarbu kufikiria kuhusu maisha ya Kiboko. Ni mtu mzima lakini amejaa michezo ya ujana. Anafuata raha. Raha ataiweza wapi? Raha nayo ni nini kama si hadaa tu? Raha ni chakula, ama raha ni mapenzi? Raha ni gari zuri au ni pesa au kazi? Raha iko wapi? Inapatikana wapi? Labda raha iko Ahera kwa wale watakaoweza. Lakini Ahera mtu atakwenda ameacha mwili unaohitaji raha yenyewe mimi mwenyewe nimekuja Lamu kutafuta raha? Labda nimekuja kupumzika tu. Raha ni mazigazi. Ni upepo upitao. Raha ni kiu isiyozimika. Kila wakati ipo ng'ambo ya pili.*
> (Dondoo 4. uk 139)

Dondoo 4 linaashiria kutokuwepo kwa raha katika maisha ya binadamu. Kila kitu ambacho binadamu hutafuta ili kimpe raha hakimpi raha anayostahili. Raha ni kitu ambacho hakifikiwi katika maisha ya binadamu. Hata ahera hakuna raha kwa sababu mtu huenda ahera bila mwili ambao unastahili kupewa raha yenyewe. Unapoifikia raha nayo husonga mbele zaidi kama mazigazi. Binadamu hapumziki kwa sababu anatafuta hela na hakuna mtu aliyepata pesa akasema ametosheka. Pesa haziletei mwanadamu raha bali humletea karaha. Kwa hivyo binadamu anastahili kuishi maisha jinsi yalivyo bila kujilazimishia mambo anayofikiria yatampa raha.

Maisha ni kama nanga. Haya ni maandishi yaliyokuwa katika leso la mwanamke mmoja wa kizungu aliyepanda chombo kimoja na Musa alipokuwa akitoka Manda kuelekea Lamu. Huu ni msemo. Kulingaa na TUKI (2014), nanga ni kitu kizito ambacho hufungwa kwenye kamba au minyororo na kuwekwa kwenye maji ili kuzuia chombo kisisonge au kuyumbayumba. Neno muhimu katika maelezo haya ni uzito. Katika msemo huu, maisha yanalinganiswa na kitu kizito. Maisha ni mazito basi ili kumzuia binadamu asiyumbeyumbe. Uzito wa maisha ndio huyapa maisha mwelekeo na kumfanya binadamu abaki kwenye mkondo ufaao.

### 4.2. Suala la Ndoa

Wanaoshikilia mtazamo wa utamaushi wanadai kuwa ndoa haina raha yoyote na kama ipo, basi ni kidogo sana. Hali ya ndoa kukosa raha imejitokeza katika riwaya ya Safari ya Lamu. Ndoa ya babake Musa, Mzee Zebu haina raha yoyote kwa sababu watu walisema kuwa yeye ni mgumba. Shida hii yeye hakuijua lakini mkewe aliijua. Ilisemekana kuwa watoto walio nao si wao bali ni wa nduguye. Jambo hili lilimfanya Mzee Zebu kuwachukia watoto hao na kila mara aliwaangalia kwa chuki sana. Mzee Zebu alikuwa na uhakika kuwa mkewe alimhasi kimapenzi. Kulingana na Fulunge (2022) ukosefu wa furaha katika ndoa au mahusiano ya kimapenzi husababishwa na uasi. Katika utafiti wa Fulunge (2022), mhusika anaweza kujiua kwa sababu amesalitiwa kimapenzi na mwenzake. Kwa hivyo kulingana na nadharia ya utamaushi, ndoa si dhihirisho la furaha katika maisha ya binadamu. Ndoa haina raha katika maisha, huweza kuwa ya matatizo yanayoweza kukatiza tamaa.

*Kila wakati baba naye alinishuku kuwa mimi si mwanawe. Lakini haya yote yalinihusu nini? Mimi sikuchaguwa atakayenizaa. Dhuluma kwangu ilikuwa ya nini? Kila siku nilipokuwa karibu naye aliniangalia kana kwamba alichunguza na kutafakari jambo ambalo halikumwelea vizuri.*
(Dondoo 5: uk 8)

Dondoo hili linaashiria hali ya kitamaushi. Ndoa ya Mzee Zubu haina furaha kwa Mzee Zebu kwa sababu kila wakati ana fikra nyingi kuhusu watoto anaowalea. Anashuku kuwa hawa watoto si wake. Jambo hili linazua chuki kwa Musa. Hii ni dalili ya mzazi aliyenunua kazi mjini Nairobi ili kujiondoa katika mazingira yanayomsababishia Mzee Zebu msongo wa mawazo. Anafanya kazi kwa bidii ili kumwonyesha mzee Zebu kuwa yeye pia ana uwezo. Hali hii nis awa na alivyoonyesha Muli (2024) kuwa katika riwaya ya Paradiso, vijana wengi wametamauka katika ndoa kwa sababu wale walio katika ndoa hawana furaha kwa sababu kuna suala la watu kuwa na wapenzi wa pembeni. Hali hii inaikosesha ndoa raha inayostahili.

Musa anaona maisha ya ndoa kama kero. Maisha ya ukapera kwake yalimpa uhuru wa kufanya lolote alitakalo. Ndoa kwake ni kama kifungo. Kama kapera ana uhuru wa kusafiri popote anavyotaka na pesa zake ni zake na hawezi kumpa mtu yeyote.

*Mawazo ya ndoa yalinitawala; je nitaiweza? Si kifungo hicho? Niliwaza. Maisha ya ukapera yalinipa uhuru kufanya lolote nilitakalo. Niliweza kusafiri popote bila ruhusa maalum. Pesa zangu zilikuwa zangu. Si lazima nimpe mtu yeyote.*
(Dondoo 6: uk 94)

Dondoo 6 linaonyesha kuwa Musa hajapenda maisha ya ndoa kwa sababu hayana raha. Ndoa kwake ni kama jela. Mtu aliye katika ndoa hana raha ya kufanya yale ayapendayo kama vile kutembea anakotaka na kutumia pesa zake jinsi anavyopenda. Katika nadharia ya utamaushi, ndoa haina raha, na kama ipo basi ni kidogo sana. Hii ndio hali inayomkumba Musa na hapendi ndoa kwa sababu ya uchache wa raha iliyomo kwenye ndoa. Hali hii inalingana na utafiti wa Chimerah (2021) ulioonyesha kuwa vijana wengi katika riwaya za Kitu Kidogo Tu! na Harusi ya Wendawazimu hawataki kujiingiza katika ndoa kwa sababu ndoa itawanyima uhuru wa kutenda mambo yao jinsi wanavyotaka.

Suala la ndoa kwa Zuleikha halina maana yoyote. Kulingana naye, ndoa ni matesa tu kwa mwanamke. Maisha ya ndoa yalimfunza na akaerevuka. Maisha ya ndoa yalimwosha akawa kama kanzu nyeupe. Aliolewa kwa miaka minne na Hamaki. Ndoa yao haikudumu kwa sababu ya hasira na mateso kutoka kwa mumewe. Alishindwa kuvumilia kwa sababu hamaki alikuwa na hasira na mwenye hasira ana uwezo wa kufanya jambo baya kwa maisha ya mwingine. Hasira kwa mwanamume ni hatari kwa usalama wa mkewe. Kwa hivyo ndoa baina ya Hasira na Zuleikha haikuwa na raha ambayo ilitarajiwa.

Katika hoteli ya Hidaya kulikuwa na kibao chenye msemo Mke ni kisu kikali chenye makali. Msemo huu una maana nzito sana katika ndoa. Kisu kikali kina madhara mabaya na hatari kwa usalama wa binadamu kwa sababu kina uwezo wa kuua. Kwa hivyo mke katika ndoa badala ya kuleta raha katika ndoa huweza kuwa na athari mbaya kwa mwanamme.

### 4.3. Suala la Kifo

Kulingana na Simiyu (2013), kifo ni hatma ya maisha ya binadamu. Maisha ya binadamu duniani ni kifo cha polepole. Katika riwaya ya Safari ya Lamu, mwandishi anaeleza kuwa kifo cha mwanadamu lazima kitokee na hakuna yeyote anayeweza kupinga kifo ikiwa kimetarajiwa kutokea. Hata mali anayomiliki mwanadamu haiwezi kuzuia kifo. Hali hii inaafiki nadharia ya utamaushi inayoeleza kuwa binadamu hana udhibiti wowote kwa maisha yake.

*Alikuwa na saa ya mkononi ambayo iliundwa kwa shaba. Alivalia maridadi. Kifo cha mwanadamu kwa Maulana hakina kukatiwa rufaa. Siku ikifika lazima uende.*
(Dondoo7, uk 20)

Kifo kinapotokea ni dhihirisho kuwa Mungu amevuna mbegu yake ambayo amepanda duniani. Kifo hutokea kwa hiari ya Mungu bali si kwa hiari ya binadamu (Simiyu, 2024). Hakuna chochote kinachoweza kuzuia kifo kutokea. Hii ndio maana katika dondoo 7, imebainika kuwa mali ya mtu haiwezi kuzuia kifo kwa sababu bwana huyu amevalia nadhifu na saa ya shaba lakini bado alikufa kwa ajali na mwili wake ulikuwa njiani kwenye lami. Kifo humpa mwanadamu fursa ya kupumzika. Petro aliaga dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu (dondoo 8).

*Petero alikuwa ameaga dunia! Ilikuwa vizuri kuwa Petero amekwenda kupumzika baada ya maradhi ya muda mrefu.*
(Dondoo 8, uk 79)

Kulingana na dondoo 8, kifo humsafirisha binadamu na kumweka mahali pazuri pa kupumzika baada ya matatizo mengi ya maisha duniani. Petero alikuwa na ugonjwa ambao haukujulikana chanzo chake. Kwa hivyo kifo kimempumzisha maumivu ambayo alikuwa akihisi. Hali hii ni sawa na maelezo ya Simiyu (2024) kuwa kifo husababishwa na Mungu ambaye humweka binadamu mahali pema. Kulingna na nadharia ya utamaushi, Mungu huyu anayesababisha kifo, aliumbwa na binadamu ili kujaribu kuelewa maana ya maisha. Kwa hivyo, kifo huashiria kuwa Mungu anavuna mbegu alizozipanda duniani.

## 5. Hitimisho

Makala hii imedhibitisha kuwa mwandishi wa riwaya ya Safari ya Lamu, John Habwe amefaulu kuwasilisha masuala ya kitamaushi katika riwaya hii. Suala la maisha limeelezwa kwa kina kuwa maisha hayana raha. Hakuna chochote ambacho binadamu anaweza kupata ili kimpe raha maishani mwake. Raha ni kama mazigazi ambayo hayafikiwi. Ukiwa karibu kufikia raha, mahitaji ya kupata raha pia husonga mbele. Suala la ndoa pia limewasilishwa kwa kina kuwa haina raha bali kuvumiliana tu. Wale wasiovumilia matatizo ya ndoa huvunja ndoa zao. Kifo kimeonyeshwa kuwa hatma ya maisha ya kila binadamu. Maisha basi ni kifo cha

polepole. Siku zinaposonga, ndipo kifo hukaribia. Kifo kimewasilishwa kama mahali pa binadamu kupumzika na kuwa na raha lakini mtu huenda ahera bila mwili ambao unastahili kupewa raha. Binadamu basi anastahili kuishi maisha jinsi yalivyo bila kutarajia maisha mazuri katika siku za baadaye.

Makala hii inapendekeza kuwa binadamu wasijitie msongo wa mawazo kwa sababu ya hali ambazo hawawezi kudhibiti. Binadamu ataishi maisha mazuri ikiwa ataishi maisha jinsi yalivyo bila kulazimisha hali yoyote. Hali hii itapunguza uwezekano wa kutokea magonjwa ya kiakili. Kwa hivyo makala hii imeonyesha uhusiano uliopo kati ya ugonjwa wa akili na fasihi andishi. Makala hii inapendekeza kuwa waandishi wa kazi za fasihi waandike kazi zenye uhalisia ili kuonyesha utamaushi katika maisha halisi ya binadamu. Kazi nyingi za kitamaushi ni za kubuni na hazitoi mfano mzuri kwa binadamu. Maudhui na wahusike wachukuliwe kutoka kwa mazingira halisi na binadamu waliowahi kuishi. Kitaaluma, makala hii inapendekeza utafiti mwingine ufanywe kuhusu hali za kitamaushi katika mazingira halisi ya binadamu.

## Marejeleo

Buliba, F. A.; Mayaka J. G & Matinde R. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

Chimerah, A. (2021), *Udhanaishi Katika Riwaya za Thomas Kamugisha: Kitu Kidogo Tu! na Harusi ya Wendawazimu*. Tasnifu ya Uzamili Katika Chuo Kikuu Cha Pwani

Fulunge, A. (2022), Matukio ya Mchakato wa Kujiua katika Riwaya ya Rosa Mistika. *Mulika*. Nambari 41 (2), 145-161 *Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Habwe, J. (2011). *Safari ya Lamu*. Nairobi, Longhorn Publishers.

Kierkegaard, S. (1849). *The Sickness unto Death.* Edited and Translated by Howard V. Princeton University Press, Princeton https://www.amazon.com

Malugu, A. & Jjingo, C. (2024). Mbinu za Kukabiliana na Utamaushi katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganisho wa Wimbo Teule wa Jux na Diamond Platnumz na Kazi Teule za Kezilahabi. *Nuru ya Kiswahili*. Juzuu 3(1), 27-42.

Muia, S. T.; Mutua, J. & Makoti, V. (2023). Usawirishaji wa Uhusika katika riwaya za Rosa Mistika na Maisha Kitendawili. Research Journal in African Languages, 4(2). Retrieved from https://royalliteglobal.com/African languages/article/view/1053.

Muli S. (2024), Athari za Udhanaishi wa Kidini kwa Vijana katika Riwaya Teule za Paradiso na Kidagaa Kimemwozea, Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

Nyimbili, F. & Nyimbili L. (2024). Types of Purposive Sampling Techniques with Their Examples and Application in Qualitative Research Studies. *British Journal of Multidisciplinary and Advanced Studies*. ISSN: 2517-276X, ISSN: 2517-2778

Ogechi, N. O. (2024), *Taratibu za Kuendesha Utafiti na Masuala Mengine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Poyi, C. J. (2021). Ishara Bwege Katika Diwani ya Kichomi. *East African Journal of Swahili Studies*, 4(1), 12-29. https://doi.org/10.37284/eajss.4.1.446.

Simiyu, F.W. (2013). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Mwanza, Serengeti Bookshop.

Simiyu, F. W. (2024). Dhana ya Kifo katika Mashairi Pepe ya Kumwomboleza Ken Walibora kwenye Kumbi za Kulikoni za Wataalam wa Kiswahili, Africa Mashariki. *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), 193-211. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1855.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. (1998). *Philosophical Labyrinth by Using Two Critical Motifs in Kezilahabis' Prose Works*. AAP 55: Swahili Forum, Vol 1, 79-91.

Wangari, M. (2019). *Ukumbi wa Lugha na Fasihi: Nadharia ya Udhanaishi*. Taifa Leo.

Wilson, V. (2011). *Research Methods: Content Analysis*. University of Saskatchewan.